



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO
AWAMU YA PILI KWA MWAKA 2020/2021**

**DODOMA
SEPTEMBER, 2021**

YALIYOMO

1.0. UTANGULIZI.....	1
2.0. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO, AWAMU YA PILI KWA MWAKA 2020/2021	2
2.1. ENEO KUU LA KWANZA: USIMAMIZI ENDELEU WA MAJI NA ARDHI	2
2.1.1. <i>Kazi zilizofanyika na matokeo kwenye maeneo ya vipaumbele.....</i>	2
2.1.1.1. Mpango wa Matumizi ya Ardhi na Usimamizi wa Mabwawa:-	2
2.1.1.2. Maendeleo ya Miundombinu ya Umwagiliaji	3
2.1.1.3. Usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji	3
2.1.1.4. Kukuza matumizi ya teknolojia ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi	3
2.2. ENEO KUU LA PILI: KUONGEZA TIJA NA FAIDA KATIKA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI	4
2.2.1. <i>Kazi zilizofanyika na matokeo kwenye maeneo ya vipaumbele.....</i>	4
2.2.1.1. Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo ya stadi.....	4
2.2.1.2. Upatikanaji bora wa pembejeo na huduma za afya ya mazao, mifugo na uvuvi.....	5
2.2.1.3. Utafiti na maendeleo.....	8
2.2.1.4. Kuimarisha na kukuza mazao ya kimkakati	9
2.2.1.5. Hali ya Usalama wa Chakula na Lishe	10
2.3. ENEO KUU LA TATU: BIASHARA NA KUONGEZA THAMANI	10
2.3.1. <i>Kazi zilizofanyika na matokeo ya Shughuli Zilizotekelezwa.....</i>	10
2.3.1.1. Kuendeleza upatikanaji wa soko kwa bidhaa zote za kipaumbele za mazao	11
2.3.1.2. Kuendeleza upatikanaji wa soko kwa ajili ya uvuvi na bidhaa za mifugo.....	13
2.3.1.3. Maendeleo ya usindikaji na kuongeza thamani.....	14
2.4. ENEO KUU LA NNE: UWEZESHI WA SEKTA, URATIBU, UFUATILIAJI NA TATHMINI	14
2.4.1. <i>Kazi zilizofanyika na matokeo ya shughuli zilizotekelezwa.....</i>	14
2.4.1.1. Sera na Mfumo wa Udhhibiti na Maendeleo ya Mazingira ya Biashara.....	15
2.4.1.2. Kuimarisha uwezo wa Vikundi na Vyama vya Ushirika	15
2.4.1.3. Kukuza na Kuimarisha Ushirikiano wa Kijinsia Katika Sekta ya Kilimo	15
2.4.1.4. Kuboresha na kuimarisha uratibu wa Programu kati ya Wizara za Kisekta na wadau 16	
2.4.1.5. Uboreshaji wa TEHAMA kwa Huduma na Mifumo ya Taarifa za Kilimo	17
2.4.1.6. Huduma za Mikopo, Ufadhili na Bima.....	18
3.0. USHIRIKI WA WASHIRIKA WA MAENDELEO: MIRADI YA MOJA KWA MOJA.....	19
4.0. USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI.....	19
5.0. MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU	20
5.1. MAFANIKIO KATIKA USIMAMIZI ENDELEU WA ARDHI NA MAJI.....	21
5.2. MAFANIKIO KATIKA KUONGEZA TIJA NA FAIDA KWENYE KILIMO, MIFUGO NA UVUVI	22
5.3. MAFANIKIO KATIKA BIASHARA NA KUONGEZA THAMANI	23
5.4. MAFANIKIO KATIKA UWEZESHI WA SEKTA, URATIBU, UFUATILIAJI NA TATHMINI.....	25
6.0. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI PROGRAMU NA HATUA ZA UTATUZI	25
7.0. HITIMISHO	28
8.0. VIAMBATISHO.....	29

VIFUPISHO

AGITF	Agricultural Inputs Trust Fund
AMCOS	Agricultural Marketing Co-operative Societies
ARDS	Agricultural Routine Data System
ASA	Agricultural Seed Agency
ASC	Agricultural Sector Steering Committee
ASCG	Agricultural Sector Consultative Group
ASDP II	Agricultural Sector Development Programme Phase II
ASLMs	Agricultural Sector Lead Ministries
ATMIS	Agriculture Trade Management Information System
CAADP	Comprehensive Africa Agriculture Development Programme
CAMARTEC	Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology
CC	City Council
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CFMAs	Collaborative Fisheries Management Areas
CPB	Cereals and Other Produce Board of Tanzania
CSA	Climate Smart Agriculture
DADPs	District Agricultural Development Plans
DC	District Council
DPs	Development Partners
FAO	Food and Agriculture Organization
GePG	Government electronic Payment Gateway
JICA	Japan International Cooperation Agency
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
MARK-UP	Market Access Upgrade Programme
MC	Municipal Council
NFRA	National Food Reserve Agency
NIC	National Insurance Corporation
NMB	National Microfinance Bank
RSs	Regional Secretariat
SACCOS	Savings and Credit Cooperatives
SAGCOT	Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania
SBT	Sugar Board of Tanzania
SIDA	Swedish International Development Cooperation Agency
SIDO	Small Industries Development Organization
TADB	Tanzania Agricultural Development Bank
TAFIRI	Tanzania Fisheries Research Institute
TAHA	Tanzania Horticultural Association
TANSHEP	Tanzania Smallholder Horticulture Empowerment and Promotion
TC	Town Council
TCD	Technical Committee of Directors

TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TIB	Tanzania Investment Bank
USAID	United States Agency for International Development
UVIKO	Ugonjwa wa Virusi vya Korona
WFP	World Food Programme
WRRB	Warehouse Receipts Regulatory Board
WRS	Warehouse Receipt System

1.0. UTANGULIZI

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (*Agricultural Sector Development Programme Phase Two - ASDP II*) inaweka msukumo kwenye maendeleo ya kilimo nchini kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo vilivyoainishwa katika mipango mbalimbali ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Malengo makuu ya Programu ni kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo (kilimo, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara zaidi na kuongeza pato la wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao, uhakika wa usalama wa chakula na lishe na kuchangia katika pato la Taifa.

Fedha zilizoainishwa kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Programu kwa miaka mitano ni shilingi **13,819,077,626,470**. Fedha hizo zimepangwa kutumika katika maeneo makuu manne ya programu ambayo ni Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji (asilimia 15); Kuongeza tija na Faida katika Kilimo (asilimia 58); Biashara na Kuongeza Thamani (asilimia 26) na Uwezesaji wa Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini (asilimia 1). Programu inatekelezwa kwa pamoja na Serikali, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi. Katika mwaka wa tatu wa utekelezaji (2020/2021), Programu ilihitaji shilingi 2,868,860,926,786.

Kwa upande wa Serikali, Programu hii inatekelezwa na Wizara sita za sekta ya kilimo (ASLMs) ambazo ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maji. Vilevile, programu inatekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Magereza na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupitia Jeshi la Kujenga Taifa.

Katika mwaka 2020/2021 Wizara za sekta ya kilimo, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilidhinishwa jumla ya Shilingi **518,873,814,934**. Aidha, katika fedha zilizoidhinishwa, Shilingi **394,438,698,386** sawa na asilimia 76 ni fedha za ndani na Shilingi **124,435,116,549** sawa na asilimia 24 ni fedha za nje.

Aidha, kiasi cha Shilingi **187,895,025,090** ziliwekezwa kupitia miradi moja kwa moja inayotekelezwa/kufadhiliwa na Washirika wa Maendeleo (DPs).

Sekta binafsi licha ya kutokuwa na makisio ya moja kwa moja katika mpango wa utekelezaji wa Programu kwa mwaka 2020/2021, ilitarajiwa kuwekeza zaidi ya shilingi bilioni 500 kwa mwaka huo kutokana mwenendo wa uwekezaji wa miaka miwili iliyopita na kuimarika kwa upatikanaji wa taarifa.

2.0. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUENDELEZA SEKTA YA KILIMO, AWAMU YA PILI KWA MWAKA 2020/2021

Katika mwaka 2020/2021 Shilingi **518,873,814,934** ziliidhinishwa kwenye bajeti za Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutekeleza maeneo makuu ya Programu zikiwa ni fedha za maendeleo (Jedwali Na. 1). Jumla ya shilingi **354,015,059,952** zilitolewa sawa na asilimia **68** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo Shilingi **312,205,727,399** zilitumika sawa na asilimia **88** ya fedha zilizotolewa.

Jedwali Na 1: Mpango na Matumizi ya Fedha kwa ajili ya Programu

Maeneo Makuu ya ASDP II	Fedha zilizopangwa			Fedha zilizotolewa kwa Mwaka			Fedha zilizotumika		
	Fedha za Ndani (Sh.)	Fedha za Nje (Sh.)	Jumla (Sh.)	Fedha za Ndani (Sh.)	Fedha za Nje (Sh.)	Jumla (Sh.)	Fedha za Ndani (Sh.)	Fedha za Nje (Sh.)	Jumla (Sh.)
Eneo Kuu la Kwanza: Matumizi Endelevu ya Ardhi na Maji	12,201,569,687	23,014,356,760	35,215,926,447	5,236,270,921	12,562,576,194	17,798,847,115	5,541,008,983	12,562,576,194	18,103,585,177
Eneo Kuu la Pili: Kuongeza tija na Faida katika Kilimo	92,839,952,655	10,092,924,112	102,932,876,767	41,061,005,328	3,675,985,782	44,736,991,109	40,574,295,113	3,675,985,782	44,250,280,894
Eneo Kuu la Tatu: Biashara na Kuongeza Thamani	276,730,093,897	75,911,374,761	352,641,468,658	254,543,700,631	28,735,253,303	283,278,953,934	221,493,915,498	20,573,813,462	242,067,728,960
Eneo Kuu la Nne: Uwezesaji wa Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini	12,667,082,147	15,416,460,916	28,083,543,063	4,583,252,651	3,617,015,142	8,200,267,793	4,282,373,024	3,501,759,343	7,784,132,367
JUMLA	394,438,698,386	124,435,116,549	518,873,814,934	305,424,229,531	48,590,830,421	354,015,059,952	271,891,592,618	40,314,134,781	312,205,727,399

Utekelezaji umefanyika kupitia miradi na kazi mbalimbali katika maeneo yote makuu; na Maeneo ya Uwekezaji ya Kipaumbele ishirini kati ya ishirini na tatu yaliyopo kwenye Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (Jedwali Na. 1, Kiambatisho 1-3).

2.1. Eneo Kuu la Kwanza: Usimamizi Endelevu wa Maji na Ardhi

Lengo la eneo hili ni kuhakikisha matumizi endelevu ya maji na ardhi kwa ajili ya mazao, mifugo na uvuvi.

2.1.1. Kazi zilizofanyika na matokeo kwenye maeneo ya vipaumbele

Baadhi ya kazi zilizofanyika na matokeo katika eneo hili ni ifuatavyo:-

2.1.1.1. Mpango wa Matumizi ya Ardhi na Usimamizi wa Mabwawa:-

- Kuratibu na kusimamia zoezi la kuandaa Mipango ya matumizi ya ardhi kwa Vijiji 47 vitakavyopitiwa na Bomba la Mafuta la kutoka Hoima nchini Uganda mpaka Tanga Tanzania.

- ii. Kuratibu na kusimamia zoezi la kuandaa Mipango ya matumizi ya ardhi kwa Vijiji 18 vilivyopo katika maeneo ya hifadhi za misitu katika Mkoa wa Kigoma.
- iii. Kuandaa mipango na matumizi ya ardhi kwa vijiji 45.
- iv. Kutolewa kwa Hati za Hakimiliki za Kimila zipatazo 28,382 katika Mikoa ya Tabora (415); Kilimanjaro (1,117); Mbeya (5,312); Simiyu (535); Njombe (306); Iringa (12,839); Kigoma (84); Lindi (316); Mara (504); Morogoro (1,404); Ruvuma (270); Pwani (358); Katavi (1,800); Shinyanga (268); Kagera (949); Rukwa (1549) na Songwe (356);
- v. Kuundwa kwa Jumuiya Tisa (9) za watumia maji katika mabonde Ziwa Tanganyika jumuiya moja (1), Bonde la Kati (2), Bondel la Pangani (1), Ruvuma (2) na Ziwa Rukwa jumuiya mbili (2). Aidha, kamati ya Kidakio moja (1) imeanzishwa katika Bodi ya Bonde ya Ziwa Rukwa;

2.1.1.2. Maendeleo ya Miundombinu ya Umwagiliaji

- i. Ujenzi na ukarabati wa skimu za Msolwa ujamaa na Njage (Kilombero), Kigugu (Mvomero), Mvumi na Shamba la mbegu la Kilangali (Kilosa) umekamilika;
- ii. Mfereji mkuu wa skimu ya umwagiliaji Msesule ya Mbarali DC umechimbwa Kilomita 3 na kusakafiwa mita 60;
- iii. Ukarabati wa skimu za Gwiri (Mbarali DC); Mkungwe, Sanga mabuni, na Kigole zote (Mbinga DC) umefanyika. Ukarabati wa skimu za ndorobo na Mkombozi za Iringa DC pia umeendelea kufanyika;
- iv. Ukarabati wa malambo 2 ya Vijiji vya Sangambi (Chunya DC) na Bugango (Missenyi DC) umefanyika;
- v. Ukarabati wa Bwawa la kufugia samaki la Kihesa kilolo (Iringa MC) umefanyika. Ujenzi wa Mabwawa 2 ya kufugia samaki ya Kashambya (Missenyi DC) na Ngage (Simanjiro DC) umefanyika;

2.1.1.3. Usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji

Wakulima wamefundishwa kuhusu usimamizi wa ghala na matumizi ya teknolojia bora baada ya mavuno ya mpunga katika miradi mitano ya umwagiliaji.

2.1.1.4. Kukuza matumizi ya teknolojia ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi

- i. Katika utekelezaji wa programu Endelevu ya Usimamizi wa Vyanzo vya maji na ardhi kati mabonde madogo ya Zigi na Ruvu, Serikali imewakutanisha wadau wa rasilimali za misitu kujadili changamoto na fursa

zilizomo kwenye rasilimali za misitu katika mabonde madogo ya Zigi na Ruvu.

- ii. Uratibu wa shughuli za uhamasishaji wa matumizi ya mwongozo wa Climate Smart Agriculture (CSA) kwa Halmashauri 5 za Mkoa wa umefanyika;

2.2. Eneo Kuu la Pili: Kuongeza Tija na Faida katika Kilimo, Mifugo na Uvuvi

Lengo la eneo hili ni kuongeza kiwango cha uzalishaji wenye tija ambapo mkulima atatumia eneo na gharama ndogo kupata mavuno mengi zaidi, kupata soko na kuimarisha mnyororo wa thamani za bidhaa.

2.2.1. Kazi zilizofanyika na matokeo kwenye maeneo ya vipaumbele

Kazi zilizofanyika na matokeo ni kama ifuatavyo:

2.2.1.1. Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo ya stadi

Katika eneo hili la kipaumbele kazi zilizofanyika ni pamoja na kuanzishwa kwa mashamba darasa, mafunzo kwa wakulima na maafisa ugani na ukarabati wa kituo cha mafunzo.

(a) Uanzishwaji na uendelezaji wa mashamba darasa

- i. Mafunzo kuhusu uzalishaji, uhifadhi na matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi kibaiolojia yametolewa katika Halmashauri za Ludewa, Wanging'ombe, Njombe na Makete kwa wakulima viongozi 200 na Maafisa 32 ngazi ya kata wakiwemo Maafisa Ugani, Maafisa maendeleo ya jamii, Watendaji wa Kata na Madiwani. Aidha, mashamba darasa 16 yameanzishwa;
- ii. Wakufunzi na maafisa ugani 131 wamepata mafunzo kuhusu udhibiti wa sumukuvu na namna ya uanzishwaji wa mashamba darasa.
- iii. Vishamba vya mfano (Demo plots) zaidi ya 200 vimeendeshwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam (1), Halmashauri za Manispaa ya Musoma (5), Iringa (3), Halmashauri ya Mji Njombe (6) na Halmashauri za Wilaya za Kwimba (10), Makete (6), Mbeya (1), Mbulu (24), Misungwi (15), Tarime (75), na Wanging'ombe (52), Chalinze (4) na Mkinga (3);
- iv. Mashamba Darasa zaidi ya 600 yameanzishwa na kuendeshwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Halmashauri za Nzega TC (3), Hai DC (6), Kigamboni MC (4), Mkalama DC (78), Momba DC (8), Nyasa DC (19), Songea MC (123), Tunduru DC (20) na Mtwara MC (3);
- v. Maeneo 320 ya kufundishia kwa vitendo kilimo bora cha mpunga na kutoa mafunzo kwa wakulima 2,560 kutoka miradi 40 ya umwagiliaji katika mikoa

ya Ruvuma, Mbeya, Manyara, Dodoma, Kilimanjaro, Pwani na Morogoro juu ya matumizi ya mbolea, mbegu zilizoboreshwa na madawa ya kuulia wadudu waharibifu yameanzishwa;

(b) Uwezeshaji kwa maafisa ugani

- i. Kuandaa Mwongozo kwa Maafisa Ugani na Wakufunzi kuhusu Tafsiri na Matumizi ya Huduma na Taarifa za Hali ya Hewa ili kuwaelimisha wakulima namna ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi;
- ii. Maafisa ugani wameendelea kupatiwa mafunzo wezeshi kuhusu masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja Kilimo Hifadhi (wanne), teknolojia bora za kilimo (982), kilimo bora cha michikichi (89) na mafunzo mengine rejea (24), Aidha mafunzo ya kilimo bora cha michikichi ilihusisha pia wanafunzi 12 wa vyuo vikuu na sekondari na vijana 1,100 wa JKT Bulombora katika mkoa wa Kigoma.
- iii. Vitendea kazi vya shughuli za Ugani kama vile (gum boots, dog catchers, dog muzzles na kits (syringes) vimetolewa kwa Maafisa Ugani 190 wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Halmashauri za Wilaya za Newala na Njombe na Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Aidha, Pikipiki 16 zilinunuliwa kwa ajili ya Maafisa Ugani wa Halmashauri za Ifakara TC (2), Masasi TC (1), Mbinga DC (6), Mkuranga DC (2), Muleba DC (1), Njombe TC (3), Tanganyika DC (1).
- iv. Ukarabati wa ndege inayotumika kunyunyiza viuatilifu katika kituo cha kilimo anga Arusha umekamilika;
- v. Maafisa uvuvi watano (5) wamewezeshwa kujiunga na masomo ya shahada ya Uzamivu kuhusu fani ya uvuvi katika vyuo mbalimbali nchini;

2.2.1.2. Upatikanaji bora wa pembejeo na huduma za afya ya mazao, mifugo na uvuvi

Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021, huduma mbalimbali zimepatikan ikiwa ni pamoja na mbolea, viutilifu; huduma za uhimilishaji na udhibiti wa magonjwa ya mifugo na uboreshaji huduma za ufugaji samaki na uvuvi.

(a) Uzalishaji na Upatikanaji wa mbegu bora za mazao ya kilimo

- i. Ugunduzi wa aina bora za Mchicha-5, Nyanya-6, Mnavu-5, Ngogwe-2, na Figiri/Loshuu-2) ambazo zinatumiwa katika maeneo mengi ya Tanzania umefanyika;
- ii. Kuimarishwa kwa benki ya mbegu ya Madiira Arusha ambapo aina 300 za mbegu zimehifadhiwa. Lengo la kuwa na benki ya Mbegu ni kuhakikisha upatikanaji wa mbegu wakati wa majanga kama vile mlipuko wa magojwa na mafuriko;

- iii. Hadi Juni 2021, tani 50,589.43 za mbegu bora zimepatikana. Kati ya hizo, tani 27,330.37 zimezalishwa nchini, tani 15,758.92 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na tani 7,500.14 ni bakaa ya msimu 2019/2020;
- iv. Uzalishaji na kusambaza vipando 13,568,422 vya mazao mbalimbali umefanyika. Hii ni pamoja na muhogo (pingili 4,766,501); viazi vitamu (vikonyo 1,833,486); maembe (miche 15,765); parachichi (miche 15,891); minazi (miche 1,072,308); mipapai (miche 57,883); mkonge (miche 2,896,000); miwa (miche 1,515,652); zabibu (miche 9,000); michikichi (miche 1,370,133); na pareto (miche 15,803);
- v. Kukamilisha ujenzi wa maabara ya kuhakiki ubora wa mbegu na ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya Wakala wa Mbegu (ASA) ikiwemo trekta 2, Mashine 2 za kupandia (Planters), Mashine 2 za kunyunyizia viuatilifu (Boom sprayers) na mashine ya kulainisha udongo (Rotavator);
- vi. Kuidhinishwa kwa matumizi ya aina mpya za mbegu 28. Mbegu hizo ni migomba (4), mtama (2), viazi vitamu (2), miwa (6), maharage (10), fiwi/ngwara (2), mahindi (1) na mpunga (1). Pia kumefanyika ugunduzi wa mbegu za miwa zinazotegemea mvua ambazo ni nafuu kwa wakulima ikilinganishwa na mbegu za awali zinazotegemea kilimo cha umwagiliaji;
- vii. Uzalishaji wa tani 481.73 za mbegu bora za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta;
- viii. Ukaguzi wa hekta 3,977.7 za mashamba ya mbegu, ghala 68 za mbegu na maduka ya mbegu 787 katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Mashariki na Pwani ili kudhibiti ubora wa mbegu zinazouzwa kwa wakulima;
- ix. Uidhinishwaji wa sampuli 1,981 za mbegu kati ya sampuli 2,533 zilizopimwa.

(b) Upatikanaji wa mbolea na viuatilifu

- i. Kusajiliwa kwa wafanyabiashara wapya 387 na kuhuisha usajili wa wafanyabiashara 533 na hivyo kufanya jumla ya wafanyabiashara wa mbolea waliopewa leseni nchini kuwa 920;
- ii. Uchambuzi wa sampuli 538 za viuatilifu umefanyika ambapo sampuli 522 sawa na asilimia 97 zimekidhi viwango. Zoezi hili limeenda sambamba na utoaji vibali 1,456 kwa wafanyabiashara wa viuatilifu nchini ambapo vibali 705 ni vya uagizaji, 176 vya uuzaji, 97 vya usajili, 24 vya ufukizaji, 13 uingizaji wa viuatilifu na 441 vya uingizaji wa shehena za mimea na mazao.
- iii. Kufanyika ukaguzi wa kampuni moja (1) na maduka 104 ya viuatilifu katika mikoa ya Mbeya, Katavi, Njombe, Songwe, Rukwa, Ruvuma, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Mara, Arusha, Mtwara, Lindi, Dar es Salaam na Kilimanjaro. Ukaguzi huo umebaini maduka 25 yanauza viuatilifu

visivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria na hivyo wamiliki wa maduka hayo kufunguliwa mashauri mahakamani.

(c) Uboreshaji mbari na udhibiti wa magonjwa ya mifugo

- i. Jumla ya kambi 22 za uhimilishaji zimeanzishwa kwenye Halmashauri mbalimbali na kuwezesha kuhimilisha ng'ombe 6,256 ikiwa ni pamoja ng'ombe 731 waliohimilishwa katika Halmashauri za Chunya DC (242), Maswa DC (320), Mwanza CC (169);
- ii. Madume bora 6 majike bora watano wamenunuliwa na kusambazwa kwa Wafugaji katika Halmashauri ya Missenyi DC;
- iii. Ukarabati wa majosho 17 ya Halmashauri za Mbarali DC (3), Simanjiro DC (8), Morogoro MC (1), Ushetu DC (1), Bukombe DC (2), Missenyi DC (1), Moshi DC (1) umekamilika. Ujenzi wa majosho 3 ya Halmashauri za Mufindi DC (2) na Tabora MC (1) umekamilika;
- iv. Dozi za chanjo 61,741,348 za magonjwa mbalimbali zimezalishwa ikiwa ni pamoja na mdomo (61,440,329), homa ya mapafu (182,055), kutupa mimba (2,456) na kimeta (116,508). Aidha matayarisho ya utengenezaji wa chanjo ya ugonjwa wa homa ya midomo na miguu umeanza;
- v. Uchanjaji wa mifugo umefanyika katika Halmashauri mbalimbali nchini ambapo Ng'ombe 1,078,689 Mbuzi/kondoo 313,407, Nguruwe 3200 na Kuku 61,485 wamepatiwa chanjo;
- vi. Usambazaji wa dawa za kuogeshea mifugo lita 1088.75 kwenye halmashauri sita za mkoa wa Arusha (Arusha DC, Meru, Karatu, Longido, Monduli na Ngorongoro) umefanyika. Aidha, lita 859.25 za dawa ya kuogeshea aina ya paranex yenye ruzuku ya serikali imepokelewa na kusambazwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika Mkoa wa Singida na ufuatailaji wa matumizi sahihi ya dawa unaendelea.

(d) Uboreshaji huduma za ufugaji samaki na uvuvi

- i. Ujenzi wa jengo la ofisi za Usimamizi wa Maeneo ya Mwambao (Beach Management Unit) katika Halmashauri ya Wilaya Mkinga umekamilika;
- ii. Doria zimeendelea kufanyika katika maziwa makuu na maji madogo;
- iii. Ukarabati wa jengo la utawala, jengo la kuzalisha vifaranga (Hatchery) na jengo la mlinzi umekamilika katika Kituo cha Ukuzaji wa Ufugaji samaki Kingolwira;
- iv. Vituo vitatu (3) vya ukuzaji viumbe maji (Kingolwira - Morogoro, Ruhila - Songea na Mwamapuli – Igunga) vimewezeshwa miundombinu ya uzalishaji wa vifaranga na kuzalisha vifanga 1,610,652;

- v. Katika kituo cha Rubambagwe ujenzi wa majengo ya nyumba tatu (3) za watumishi, jengo la utawala, hosteli na jengo la kuzalishia vifaranga vya samaki pamoja na uchimbaji wa mabwawa unaendelea;
- vi. Vifaranga 5000 wa samaki wamenunuliwa na kusambazwa kwa Wafugaji wa samaki wa Iringa MC (3000) na Itilima DC (2000);
- vii. Ujenzi wa maabara ya uvuvi TAFIRI umekamilika kwa asilimia 96;
- viii. Ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi (The Marine Park and Reserves Unit - MPRU) Tanga zimekamilika. Ujenzi wa jengo la ofisi la MPRU Mafia umefikia asilimia 25;
- ix. Ununuzi wa watoto wa samaki (fingerlings) 40,000 na kusambazwa kwa wafugaji wa samaki umefanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo;
- x. Jumla ya Maeneo 12 ya Ushirika wa Usimamizi wa Uvuvi (Collaborative Fisheries Management Areas - CFMAs) yametambuliwa na kuanzishwa katika wilaya tano za majaribio zinazotekeleza Mradi wa SWIOFish ambazo ni Halmashauri za Wilaya za Mkinga (2), Pangani (3), Bagamoyo (3) na Lindi Vijijini (3) na Halmashauri ya Jiji la Tanga (1);
- xi. Miongozo saba ya ufugaji samaki imepitwa. Miongozo hiyo ni Mwongozo wa ufugaji wa Samaki kwenye vizimba; Mwongozo wa Uzalishaji wa vifaranga vya Samaki na Usimamizi wa vitotoleshi; Mwongozo wa Usimamizi wa Bwawa; Mwongozo Kilimo cha Kaa; Mwongozo wa Udhhibiti wa Magonjwa ya Samaki; Mwongozo wa Kilimo cha Mwani na Mwongozo wa utengenezaji wa Chakula cha Samaki.

2.2.1.3. Utafiti na maendeleo

- i. Ugunduzi wa mbegu mpya za mazao 10 umefanyika na zipo kwenye hatua za uchunguzi kuangalia tabia na ufanisi wake. Mbegu hizo ni za maharage, choroko, miwa, ndizi, karanga, mtama, uwele, ngano, mahindi na mpunga;
- ii. Utafiti wa wingi wa samaki aina ya Jodari na jamii yake katika ukanda wa Pwani wa Tanzania Bara na tathmini ya samaki wa tabaka la juu la maji umefikia umekamilika. Aidha, ukusanyaji wa takwimu za kibaiolojia za samaki aina ya Pweza katika Mikoa ya Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara umekamilika;
- iii. Utambuzi wa wabunifu na watengenezaji 12 wa zana za kilimo katika mikoa ya Manyara, Dodoma, Shinyanga, Mwanza, Arusha, Njombe na Tanga kwa lengo la kuwaunganisha na taasisi za teknolojia za CAMARTEC na SIDO ili kuboresha ufanisi wa zana hizo kuendana na soko umefanyika. Zana zilizobuniwa ni pamoja na mashine ya kuchakata mkonge, mashine ya kupura mahindi, mashine ya kukata michembe, mashine ya kupanda ngano na ufuta inayokokotwa na wanyamakazi, mashine ya kubangua karanga,

- mashine ya kuchakata mkonge, pampu za kumwagilia maji mashambani na trekta;
- iv. Ukaguzi na usimamizi wa usambazwaji wa Teknolojia za kisasa katika uzalishaji kwenye maeneo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika Halmashauri za Manispaa zote tano za Mkoa wa Dar es Salaam umefanyika;

2.2.1.4. Kuimarisha na kukuza mazao ya kimkakati

(a) Mazao Makuu Asilia ya Biashara

Katika mwaka 2020/2021 mikakati ya uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ya Tumbaku, Pamba, Kahawa, Chai, Pareto, Korosho na Miwa imeendelea kutekelezwa:

(b) Mazao ya Mafuta

Uzalishaji wa mbegu 3,824,508 za chikichi na usambazaji wa miche 10,200 katika Mikoa ya Kigoma, Katavi, Kagera, Rukwa, Mbeya, Pwani na Ruvuma umefanyika.

(c) Mazao ya Bustani

Uhamasishaji wa vijana kuzalisha mazao ya bustani na matumizi ya teknolojia za kisasa za uzalishaji wa mazao hayo umefanyika. Aidha, mafunzo ya kanuni bora za kilimo na matumizi ya mbolea kwa zao la migomba kwa Maafisa Ugani 11 na wakulima 85 wa Wilaya za Rombo na Moshi Vijijini yamefanyika. Mbegu bora za mchicha tani 1.376 zikiwemo mbegu za awali tani 0.25 na za msingi 1.126 zimeshalishwa.

(d) Mazao ya Chakula

Uzalishaji wa mazao ya chakula ikiwemo: mahindi, mpunga, mtama/uwele, ngano, mikunde, ndizi, muhogo na viazi umeendelea kuongezeka kama ifuatavyo:

Zao la Mpunga

Uhamasishaji wa matumizi ya kanuni bora za kilimo, teknolojia bora za uzalishaji, usimamizi baada ya kuvuna pamoja na uimarishwaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

Aidha, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kupitia Mradi wa Kupunguza Upotevu na Kuimarisha Mnyororo wa Thamani wa Zao la Mpunga imetoa mafunzo ya usimamizi wa mpunga baada ya kuvuna kwa Maafisa Ugani 563 kutoka

Mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Manyara, Kilimanjaro, Mwanza, Rukwa na Dodoma.

Zao la Muhogo

Mkakati wa Miaka Kumi (10) wa Uendelezaji wa zao la Muhogo (2020-2030) umezinduliwa. Mkakati huo umelenga kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani milioni 8.2 mwaka 2019 hadi tani milioni 24 mwaka 2030 na tija kutoka tani 8.3 kwa hekta hadi tani 16 kwa hekta ifikapo 2030.

mafunzo kuhusu udhibiti wa magonjwa ya batobato na michirizi ya kahawia kwa yametolewa kwa wakulima 238 katika Wilaya za Mkuranga, Muheza, Bagamoyo, Mkinga, Sengerema, Bunda, Mtwara vijijini na Nyasa.

2.2.1.5. Hali ya Usalama wa Chakula na Lishe

Uimarishaji wa hifadhi ya chakula nchini umeendelea ambapo tani 58,813.401 za nafaka zikiwemo tani 51,832.502 za mahindi, 850.908 za mtama na tani 6,129.991 za mpunga zimenunuliwa na kuhifadhiwa. Kiasi hiki kimwezesha Hifadhi ya Taifa ya Chakula kufikia tani 107,384.057.

Mwongozo wa kutekeleza masuala ya lishe katika kilimo umeandaliwa ambapo mafunzo kuhusu mwongozo huo yametolewa kwa wadau 185 wa kilimo na lishe katika Mikoa ya Singida, Shinyanga na Manyara.

2.3. Eneo Kuu la Tatu: Biashara na Kuongeza Thamani

Eneo hili lina lenga kutatua vikwazo vya upatikanaji wa masoko ya uhakika kwa wakulima na kuongeza thamani ya mazao. Hii ni pamoja na: (i) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika kilimo-biashara; (ii) Kuboresha mifumo ya kudumu ya masoko (iii) Kuboresha miundombinu ya masoko ikiwemo barabara za vijijini na maghala (iv) Upatikanaji wa taarifa za uhakika za masoko (v) Kuhamasisha usindikaji na uongezaji wa thamani katika mazao.

2.3.1. Kazi zilizofanyika na matokeo ya Shughuli Zilizotekelezwa

Kazi mbalimbali zimefanyika katika jumla ya maeneo yote matatu ya vipaumbele katika uwekezaji kwenye eneo kuu la Biashara na Kuongeza Thamani kama ifuatavyo: -

2.3.1.1. Kuendeleza upatikanaji wa soko kwa bidhaa zote za kipaumbele za mazao

Kazi kubwa zilizofanyika ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara vijijini; kuendeleza upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo kama inavyoainishwa: -

a) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara na masoko

- i. Matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 10,750.97 yamefanyika katika Halmashauri mbalimbali nchini. Maandalizi ya Ujenzi wa barabara za lami 73.6km kwenye Halmashauri zinazotekeleza mradi wa Agri-Connect umefanyika. Aidha, kazi za ukamilishaji wa ujenzi wa barabara zinaendelea ambapo kilometa 81.63 zipo kwenye hatua mbalimbali za ukamilishaji na ujenzi wa kilometa 12.2 umekamilika kwa kiwango cha lami kwenye Halmashauri ya Rungwe;
- ii. Ujenzi wa vihenge vya kisasa (Silos) Babati (Manyara), Shinyanga, Songea (Ruvuma), Makambako (Njombe), Mbozi (Sogwe) Sumbawanga, Mpanda (Katavi) na Dodoma kupitia Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Kuhifadhi wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula umefikia asilimia 82.7. Aidha, malipo kwa Mkandarasi na Mshauri Elekezi wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhi korosho yamefanyika;
- iii. Usanifu wa ujenzi wa ghala 14 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 hadi 3,000 za mazao unaendelea;
- iv. Ujenzi wa miundombinu ya ghala tano (5) inayolenga kuboresha uhifadhi na kurahisisha upatikanaji wa taarifa na masoko ya mchele katika katika skimu za Msolwa Ujamaa (tani 1,700), Njage (tani 1,700), Mvumi (tani 1,300), Kigugu (tani 1,000), na Mbogo Komtonga (tani 1000) umekamilika;
- v. Ujenzi wa Soko la Samaki Mbamba Bay-Ziwa Nyasa; Ujenzi wa Mwalo wa Ihale (Busega) na Igabiro; Ukarabati wa Mwalo wa Kayenze (Ilemela), Igombe (Ilemela), Chifunfu/Kijiweni (Sengerema) na Kisorya (Bunda) umekamilika;
- vi. Ujenzi wa mabanda mawili ya kukusanyia majani Chai katika Kijiji cha Iboya (Njombe TC) umekamilika. Ujenzi wa masoko ya mazao ya Holili (Rombo DC), Soko la matunda na mbogamboga la Dongobesh (Mbulu DC), ujenzi wa choo cha soko la mazao la Kibaya (Kiteto DC) na soko la mazao la Karatu Mjini (Karatu DC) umekamilika;
- vii. Ujenzi wa soko la mazao la Nyarero (Tarime DC) umekamilika. Ujenzi wa masoko ya mazao ya Dongobesh (Mbulu DC), Holili (Rombo DC) na Karatu (Karatu DC) inaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha ukarabati

wa masoko ya mazao ya Kantawa (Nkasi DC), Majengo (Tunduma TC) na Mbulu DC umekamilika;

b) Kuendeleza upatikanaji wa masoko ya mazao

- i. Ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko ya mazao ya chakula kutoka mikoa 26 umefanyika. Taarifa hizi zinajumuisha pia taarifa za masoko ya mifugo na mazao ya mifugo kutoka Wilaya 53;
- ii. Bodi ya Sukari imeunganisha mfumo wa *SBT mobile application* na mfumo wa utoaji vibali wa *ATMIS*. Pia, Bodi imeunganisha mfumo wa *ATMIS* na mfumo wa makusanyo ya fedha za Serikali (Government Electronic Payment Gateway – GePG) ili kurahisisha utoaji wa namba za malipo (Payment Control Numbers) na kuboresha huduma kwa wateja. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority - TRA) imedhibiti sukari iendayo nje ya nchi “On Transit Sugar” kwa kutumia mfumo wa *Cargo Tracking System* ambao umesaidia sukari hiyo isibaki nchini na kuharibu soko la sukari;
- iii. Uratibu wa minada 70 ya uuzaji wa korosho umefanyika ambapo tani 206,718.880 za korosho ghafi zenye thamani ya Shilingi 473,178,774,764 zimeuzwa. Kati ya hizo, daraja la kwanza, bei ya juu ya korosho ilikuwa Shilingi 2,707 na bei ya chini ilikuwa Shilingi 1,685; na kwa daraja la pili bei ya juu ilikuwa Shilingi 2,300 na bei ya chini ilikuwa Shilingi 1,300;
- iv. Katika msimu wa 2020/21, Bodi ya Tumbaku imetoa vibali vya kuuza tani 20,381.4362 za tumbaku zenye thamani ya Dola za Marekani 74,850,850 nje ya nchi ikilinganishwa na tani 70,824.21 zilizouzwa msimu wa 2019/20;
- v. Katika msimu wa 2020/21, kumefanyika ununuzi wa maua ya pareto kwa bei elekezi ya Shilingi 2,500 kwa kilo ikilinganishwa na Shilingi 2,400 ya msimu wa 2019/20. Hata hivyo, bei ya juu ya maua imeongezeka ilifikia Shilingi 4,000 kwa kilo. Bidhaa zilizouzwa nje ya Nchi zenye thamani ya Shilingi bilioni 11 ni pamoja na Utomvu (crude extract), Dawa (dried marc), na Poda (powder) (Jedwali Na. 9);
- vi. Katika msimu wa 2020/21, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) imenunua tani 2,695.24 za mahindi ambazo zilizalisha unga tani 2,156.192 na pumba tani 539.048. Aidha, katika kipindi hicho tani 719.46 za alizeti zilikamuliwa katika kiwanda cha Kizota Dodoma na kuzalisha lita 215,838 za mafuta ya alizeti na tani 503.622 za mashudu. Aidha, katika msimu huo, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) umenunua tani

58,813.401 za nafaka zikiwemo tani 51,832.502 za mahindi, 850.908 za mtama na tani 6,129.991 za mpunga, alizeti tani 85.06, mtama tani 988.83 na maharage tani 3.64;

- vii. Tani 52,772 za kahawa safi zimeuzwa ambayo ni sawa na asilimia 81 ya makusanyo ya kahawa katika msimu husika;
- viii. Tani 8.5 za chai kavu ziliuzwa nje ya nchi kwa wastani wa Dola za Marekani 1.37 kwa kilo ambapo thamani ya mauzo yote ni Dola za Marekani 11,697,720. Pia, tani 7.8 ziliuzwa katika soko la ndani kwa wastani wa Shilingi 9,023 ambapo mapato yalikuwa Shilingi 16,198,395.077.

2.3.1.2. Kuendeleza upatikanaji wa soko kwa ajili ya uvuvi na bidhaa za mifugo

Hili ni eneo mahsusi la kipaumbele katika uwekezaji kwenye sekta ya mifugo na uvuvi. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa machinjio na minada katika sehemu mbalimbali nchini.

a) Ujenzi na ukarabati wa machinjio

- i. Ujenzi wa Machinjio ya kisasa Vingunguti (Ilala CC) na machinjio ya kawaida (slaughter house) Mafinga Mji umekamilika. Aidha, ujenzi wa machinjio ya Mabwepande katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Ng'ombe katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Ubaruku katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na Mabunda katika Halmashauri ya Wilaya ya Muleba unaendelea;
- ii. Ukarabati wa Machinjio 21 kwenye Halmashauri mbalimbali nchini kama vile Butiama DC (1), Mbulu TC (1), Tarime TC (1), Rungwe DC (2), Njombe TC (1), Igunga DC (1), Kilolo DC (1), Bukoba MC (1), Moshi DC (1), Mwanga DC (1), Pangani DC (1) umekamilika. Ukarabati wa machinjio unaendelea katika Halmashauri mbalimbali ikiwa ni pamoja na Korogwe, Muleba na Bariadi;
- iii. Ujenzi wa Mnada wa mifugo wa Ngogwa (Kahama MC), ukarabati wa minada 4 ya Igingilanyi, Kimande, Igula na Nyang'oro (Iringa DC) umekamilika.

b) Ujenzi na ukarabati wa minada

- i. Ujenzi na ukarabati wa minada ya Ipuli, Igunga, Nata na Murusagamba umekamilika. Ujenzi wa mnada wa upili wa Buzirayombo umeendelea na

kazi imefikia 40%. Mnada wa mpakani wa Mtukula umefanyiwa upembuzi yakinifu, mchoro umeandaliwa na gharama za ujenzi zimekadiriwa;

- ii. Ujenzi wa Mnada wa mifugo wa Ngogwa (Kahama MC), ukarabati wa minada 4 ya Igingilanyi, Kimande, Igula na Nyang'oro (Iringa DC) umekamilika.

2.3.1.3. Maendeleo ya usindikaji na kuongeza thamani

- i. Ujenzi wa Kongano la Kuendeleza Sekta ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi jijini Dodoma unaendelea ambapo msingi wa kongano umeshakamilika;
- ii. Mashine mbili za kukoboa na kusaga nafaka zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima wa Missenyi DC (1) na Moshi MC (1);
- iii. Mashine moja ya kukamua mbegu za mafuta (oil extracting machine) imenunuliwa na kusambazwa kwa Wakulima wa Missenyi DC;
- iv. Mafunzo ya uchunaji ngozi kwa wakaguzi wa ngozi 27 kutoka Mikoa ya Dar es salaam (6), Morogoro (10) na Pwani (11) yamefanyika;
- v. Wakaguzi wa ngozi 113 wameteuliwa, wachunaji 810 wamepatiwa mafunzo ya uchunaji bora wa ngozi na kupatiwa zana za kufanyia kazi. Aidha, vitambulisho 120 vimetengenezwa na vitambulisho 34 tayari vimegawiwa kwa wapanga madaraja ya Ngozi;
- vi. Viwanda viwili vya kuchambua pamba vilivyo chini ya Chama Kikuu cha Ushirika Chato (Geita) na Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (Shinyanga) vimefufuliwa na kuanza kufanya kazi.

2.4. Eneo Kuu la Nne: Uwezeshi wa Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini

Eneo hili linalenga kuweka mazingira wezeshi ya Sekta ya kilimo, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini. Hii ni pamoja na: (i) Kupitia sera na miongozo inayoweka mazingira wezeshi ya biashara kwenye sekta ya kilimo; (ii) Kuboresha na kuimarisha uratibu wa sekta; (iii) Kuimarisha mifumo ya tathmini na ufuatiliaji wa Sekta ya kilimo; (iv) Kuboresha uwezo na mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa takwimu za kilimo; (v) Kujenga uwezo katika ngazi zote; (vi) Kuboresha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa ajili ya Kilimo; (vii) Kuimarisha huduma za Kifedha; na (viii) Kuimarisha ushiriki wa jinsi zote kwenye shughuli za kilimo.

2.4.1. Kazi zilizofanyika na matokeo ya shughuli zilizotekelezwa

Kazi zilizofanyika na matokeo katika eneo kuu la Kuwezesha Sekta, Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini zimelenga kwenye maeneo saba ya kipaumbele ya uwekezaji ambapo maeneo na baadhi ya kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:-

2.4.1.1. Sera na Mfumo wa Udhhibiti na Maendeleo ya Mazingira ya Biashara

- i. Chambuzi mbalimbali zimefanyika ikiwa ni pamoja na Utekelezaji wa Makubaliano ya Malabo (Tanzania performance in the 2016-2017 Biennial Review Report on Implementation of CAADP Malabo Declaration), Utafiti na Uchambuzi wa Mnyororo wa thamani wa zao la Parachichi (Avocado Value Chain Analysis in Tanzania), Uchambuzi wa Bajeti ya Sekta ya Kilimo na Changamoto ya Utekelezaji (Analysis of Agriculture Sector Budget Implementation and Challenges); na Uchambuzi wa Mfumo wa Uagizaji wa Mbolea ya Pamoja (Review of the Fertilizer Bulk Procurement System), Utambuzi wa teknolojia na ubunifu wa zana za kilimo (Mapping Agricultural Innovations and Technologies and Dissemination through Coaching or Stakeholders Engagement);
- ii. Upitiaji wa Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013 na kuandaa Mkakati wa utekelezaji kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika sekta ya kilimo;

2.4.1.2. Kuimarisha uwezo wa Vikundi na Vyama vya Ushirika

- i. Ukaguzi wa Vyama 507 vya Ushirika umefanyika katika Halmashauri za Bumbuli DC(31), Chamwino DC (12), Hai DC(17), Kigamboni MC (10), Kilindi DC(3), Kisarawe DC (4), Kyerwa DC(30), Makambako TC(6), Mbarali DC(35), Mbinga DC (74), Mbinga TC(1), Momba DC(4), Msalala DC(42), Ngorongoro DC(4), Songea MC(30);
- ii. Vyama 77 vimesajiliwa katika Halmashauri za Arusha CC (2), Ifakara TC (7), Kigamboni MC (10), Kilosa DC(1), Makete DC(1), Pangani DC (2), Ubungo MC (50), Kibaha TC(4);
- iii. Uhamasishaji wa vikundi kuanzisha ushirika; Kusimamia na kudhibiti vyama; Kutoa elimu ya ushirika, Kufuatilia madeni sugu; Kuhamasisha vyama kununua pembejeo kwa pamoja; Kusimamia na kufuatilia matumizi bora ya rasilimali umefanyika Mkoani Iringa;

Harakati hizi zimewezesha pamoja na mambo mengine kuongezeka kwa thamani ya hisa na akiba za wanachama kwenye Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 819 mwaka 2019/2020 hadi Shilingi bilioni 891 mwaka 2020/2021.

2.4.1.3. Kukuza na Kuimarisha Ushirikiano wa Kijinsia Katika Sekta ya Kilimo

Serikali kushiriki katika uratibu wa utekelezaji wa miradi na programu zinazotekelezwa Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha masuala ya jinsia yanazingatiwa katika mipango, bajeti, mikakati na utekelezaji wa miradi kama inavyooneshwa kwenye baadhi ya miradi.

- i. Katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kushirikisha Vijana katika Kilimo (National Strategy for Youth Involvement in Agriculture –NSYIA 2016-2021), Halmashauri 48 zimetenga hekta 217,882.36 kwa ajili ya kuwezesha vijana kushiriki katika shughuli za kilimo;
- ii. Mafunzo kuhusu kilimo biashara cha mbogamboga na matunda, akiba na mikopo, uongozi; matumizi ya teknolojia za kielektroniki kwenye kupata taarifa za masoko, na programu ya uanagenzi (Apprenticeship) yametolewa kwa vijana 3,807 katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe na Iringa;
- iii. Vijana 448 wamejengewa uwezo kuhusu taratibu za kunufaika na mfuko wa maendeleo ya vijana.
- iv. Vikundi 21 vimewezeshwa kupata mikopo yenye thamani ya Shilingi 89,500,000 kutoka katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana uliopo chini ya Halmashauri za Mbeya, Songwe, Busokelo, Mbozi, Njombe, Njombe Mji, Wanging'ombe, Kilolo, Mufindi, Mafinga na Iringa.

2.4.1.4. Kuboresha na kuimarisha uratibu wa Programu kati ya Wizara za Kisekta na wadau

- i. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021 Kitengo cha Uratibu wa Programu, kiliratibu vikao saba (7) vya timu ya Waratibu (NACOTE), vikao vinne (4) vya Wakurugenzi (TCD), na Kikao kimoja cha Kamati ya Maamuzi (ASC). Aidha, kikao cha Maafisa Habari na Wakuu wa Vitengo vya Mawasiliano kwenye Wizara za Kisekta walikutana kuweka mpango kazi wa kuitangaza Programu kwa wadau kupitia Wizara na Taasisi wanazoziongoza.
